

Haki za Mteja:

Kama mshiriki katika Mpango wa ND Ryan White Sehemu ya B, una haki ya:

- Kutendewa kwa heshima, hadhi, mazingatio na huruma.
- Kupokea huduma za jamii.
- Kupokea huduma za usimamizi wa kesi bila ubaguzi kwa msingi wa mbari, rangi, jinsia/jinsi, kabila, asili ya taifa, dini, umri, tabaka, mwelekeo wa jinsia, uwezo wa kimwili na/au akili.
- Kushiriki katika kuunda mpango kwa ajili ya huduma za jamii.
- Kufahamishwa kuhusu huduma na machaguo uliyo nayo.
- Kufikia makubaliano na mhudumu wako wa jamii kuhusu muda ambao utawasiliana, iwe ni ana kwa ana au kwa njia ya simu.
- Rekodi zako za matibabu na za huduma za jamii kuhifadhiwa kwa siri.
- Kuwasilisha manung' uniko kuhusu huduma unazopokea au unazonyimwa

Majukumu ya Mteja:

Kama mshiriki katika Mpango wa North Dakota Ryan White Sehemu ya B, una jukumu la:

- Kuwaonyesha heshima na ustahifu.
- Kulinda usiri wa wateja wengine unaoweza kukutana nao kwenye shirika.
- Kutowadhulumu wala kutoa vitisho vya kimwili, kingono, matusi na/au hisia kwa wahudumu wa ajmii, wafanyakazi au wateja wengine.
- Kushiriki kulingana na uwezo wako kuunda mpango wa huduma ya jamii.
- Kumfahamisha mhudumu wako wa jamii matatizo yoyote uliyo nayo kuhusu mpango wako wa huduma ya jamii au mabadiliko katika mahitaji yako.
- Kuweka na kudumisha miadi kadri ya uwezo wako, au ikiwezekana, kupiga simu ili kusitisha au kubadilisha saa za miadi.
- Kuendelea kuwasiliana na mhudumu wako wa jamii kwa kumfahamisha kuhusu mabadiliko katika anwani au nambari ya simu, mapato yako na kujibu simu au barua za mhudumu wa jamii kadri ya uwezo wako.
- Kumpa mhudumu wako wa jamii ombi lolote la malipo ya bili ndani ya siku 30 za tarehe ya taarifa na kutoa nyaraka zinazohitajika.
- Kufuata maelekezo ya mhudumu wa jamii ili kupata usaidizi kutoka kwenye mipango na huduma zilizopo.
- Kuendelea kupata utunzaji wa kumtembelea daktari wako mara kwa mara na kunywa dawa uliyoagizwa na daktari ili kuhakikisha afya na ustawi wako.
- Kila miezi sita thibitisha tena ustahiki na uandikishaji wako katika mpango wa ND Ryan White Sehemu ya B. **Lazima ujiandikishe upya kufikia tarehe 30 Aprili na kuthibitisha upya kufikia tarehe 31 Oktoba** kila mwaka kwa ustahiki endelevu wa Ryan White.

Ninaelewa taarifa zilizo hapo juu na nimepokea nakala ya rekodi zangu.

Sahihi ya Mteja/Mlezi	Tarehe
Sahihi ya Mhudumu wa Jamii	Tarehe